

Nathanael Greene Middle School

# MIUNGANISHO

AGOSTI 19, 2022

## KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI



**DKT. JAVIER MONTAÑEZ**
Afisa Mkuu Msimamizi

Karibu kwa toleo la mwisho la Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence (PPSD) kijarida cha mara mbili kwa wiki! Ikiwa wewe au mtu unayemjua atakosa mojawapo ya majarida yetu, unaweza kupata matoleo ya awali kwenye tovuti ya Wilaya katika lugha nyingi.

Ni ngumu kuamini ya kwamba wanafunzi wetu wanarudi shuleni karibia wiki moja kutoka sasa! Nataka kusema asante kubwa, kutoka moyoni kwa wanajumuiya wetu wa Shule za Umma za Providence ambao walitoa muda wao na bidii majira haya ya joto kuhakikisha ya kwamba tunaanza mwaka wa shule 2022-23 kwa nguvu. Tuna weka kazi za maana katika miezi kadhaa iliyopita ili kuendelea kuziba pengo la maendeleo na kusaidia wanafunzi wetu kunawiri.

Tulikuwa na wanafunzi maelfu kadhaa wanao shiriki katika Mafunzo ya Majira ya Joto katika madarasa ya K-12. Hii inajumuisha Hesabu, ELA, Sayansi na Madarasa ya STEM kwa wanafunzi wadogo kiasi. Na inajumuisha upataji wa alama na mpangilio wa CTE kwa wanafunzi wetu wa shule ya upili.

Walimu wetu pia walitumia wiki kadhaa zilizopita kwa kuboresha ujuzi wao, na kufaidika kwa masaa mengi ya maendeleo ya kitaaluma kwa kila kiwango. Hii inajumuisha walimu wetu wakuu wa shule, viongozi wapya katika kiwango cha Wilaya, wakufunzi, walimu wapya na walimu wanao shiriki katika zaidi ya kozi 100 tofauti za maendeleo ya kitaaluma za kulipwa.

Aina hiyo ya kujitolea inaonyesha wanafunzi wetu na walimu wetu wanaelewa ya kwamba kujenga wilaya ya shule ambayo jumuiya yetu inastahili ni kazi ya mwaka mzima. Siwezi ngoja mwaka wa shule uanze ili niweze kuona malipo ya kazi hiyo ya bidii!

## TAARIFA MPYA ZA WILAYA

### Kurudi kwa Katikati ya Shule

Mwanzo wa mwaka mpya wa shule unaleta maswali mengi – ni wakati gani kengele hulia? Mwanafunzi wangu anahitaji aina gani ya bidaa za shule? Ni rasilimali gani zinapatikana kusaidia mwanafunzi wangu katika masomo au kuhudhuria? Tuna kushughulikia!

Tembelea **kitovu chetu cha Kurudi Shuleni** kwa majibu haya yote na zaidi. Pia utapata taarifa muhimu kuhusu ni nini kilicho kipya mwaka huu, kama vile usitishaji wa mapema kwa mwezi kwa maendeleo ya kitaaluma.

### Kurudi Shuleni Salama

Shule za Umma za Providence zitakua na **mbinu kadhaa za miongozo na upunguzaji wa COVID-19** zinazotumika kusaidia kuhakikisha kurudi shuleni kwa afya. Bofya hapa kusoma mwongozo kamili ulio sasishwa wa mwaka wa shule 2022-23, ikiwemo majaribio kwa wasio onyesha dalili, usafishaji wa hewa, mapendekezo ya barakoa na usafishaji zaidi. Wazazi wanapaswa pia kutambua kwamba wanafunzi walio peana fomu za idhini kuhusu majaribio ya COVID mwaka uliopita hawahitaji fomu nyingine ya idhini mwaka huu. Ikiwa wazazi wanapendelea kusitisha idhini ya majaribio kwa mwanafunzi wao, wanaweza kuwasiliana na muuguzi wa shule.

### Hakuna Pasi za RIPTA Zinazo hitajika kupitia Oktoba 1


Kwa ajili ya suala la uzalishaji/usambazaji, Idara ya Umma ya Usafiri ya Rhode Island (RIPTA) haitakuwa na kadi za WAVE inayopatikana kwa wanafunzi kwa wakati ufaao katika mwanzo wa shule. Kwa hivyo, RIPTA imekubalia **wanafunzi wote wa shule ya upili ya Providence** kusafiri bila pasi kuanzia 8/29 hadi 9/30. Shule za Umma za Providence zitawasilia familia hivi karibuni kuhusiana na taarifa ya pasi za kupakua kutoka mwaka uliopita na jinsi ya kuitisha pasi mpya kabla ya Oktoba tarehe 1. Familia pia zinahitaji kutafuta vipeperushi kutoka kila shule ikiwa na njia za RIPTA kufikia na kutoka kwa jengo.

### Usalama wa Shule

Usalama wa wanafunzi na wafanyakazi unakuja kwanza katika Shule za Umma za Providence. Majira haya ya joto, Wilaya ilifanya kazi na Polisi wa Providence, Idara ya Wazima Moto ya Providence, na Wakala ya Usimamizi wa Dharura ya Rhode Island kuhakiki na kusasisha Mpango wetu wa Utayari wa Dharura ya Shule. Mpango huu unaeleza majukumu ya wafanyakazi wa shule wakati wa hali kadhaa za dharura. Bofya hapa kujifunza zaidi, pamoja na ujumbe familia zina tarajia kupokea wakati kuna mifano ya usalama au hali ya dharura katika shule ya mtoto wao.


## KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo ya ajabu kila siku. Hapa kuna mifano kadhaa.




### KUPIGANA NA MOTO 101

Hiki kikundi cha maajabu cha wanafunzi chipukizi wakubwa kutoka **Shule ya Upili ya Central** walitokea katika ukurasa wa kwanza wa Jarida la Providence wakati wanapo shiriki katika akademia ya moto ya kwanza ya Wilaya! Mpango huo ulianza majira haya ya joto ikiwa na masaa 150 ya mafunzo ya kulipiwa, inaendelea mwaka wote wa shule kwa idadi ya jumla ya masaa 450 ya mafunzo! Baada ya kuhitimu, wanafunzi hawa watakuwa na nafasi ya kuingia katika Idara ya Kuzima Moto ya Providence!




### WAHITIMU WA MAFUNZO YA MAJIRA YA JOTO

Hongera kwa Darasa la 2022! Wanafunzi hawa wa maajabu wamestahiki kupokea diploma katika Mafunzo yetu ya Majira ya Joto na kuhitimu kwenye sherehe mapema mwezi huu katika PCTA. Wahitimu wametoka Wilayani kote na inajumuisha wanafunzi kutoka **360, Alvarez, Central, Classical, E-Cubed, Hope, JSEC**, na **Mount Pleasant High School**.



### MAFANIKIO YA KUOGELEA

Mwezi huu ndio mwezi wa Makutano ya Mashindano ya Kuongelea ya Jiji ya kila mwaka, ambapo wanafunzi wanao wakilisha kituo cha burudani katika jumuiya yao wanashindana dhidi ya wengine. Waokoaji majini kutoka kila jumuiya wanashindana pia, ambapo medali zinapewa kwa washindi wakuu wa 3. Mwaka huu wanafunzi wawili wa **Shule ya Upili ya Mount Pleasant** na waokaji majini wa mara ya kwanza, walishinda tuzo 3 za kwanza. Promise Seales alipata nafasi ya 3 dhidi ya waokaji majini wengine wanawake, na Bryant Agramont alishinda nafasi ya 1 kwa mwokoaji majini kwa kitengo cha wanaume.




### SHUJAA WA MTAANI

Hongera kwa mhitimu wa **Shule ya Upili ya Classical** na nyota wa kandanda wa jimbo zote, Michaela White, ambaye hivi majuzi alionyeshwa katika sehemu ya Shujaa wa Mtaani katika WPR. Majira haya ya vuli Michaela ata peleka talanta zake katika Chuo Kikuu cha Minnesota Duluth ambapo atashiriki katika kandanda na riadha! Kuwa na bahati njema, Michaela!

Tazama video: https://www.wpri.com/sports/hometown-hero-michaela-white-classical/

## KUANGAZIA WAFANYAKAZI

Pata kujua watu wa ajabu wanaofanya kazi na wanafunzi wetu kila siku!

**Sandra Grenga**
*Karani kwa Mwalimu Mkuu Msaidizi*

Aliye katika: **Nathanael Greene Middle School**

Alijiunga na PPSD mnamo: **2000**

***Je, siku yako ya kawaida katika ofisi ya shule inakuwa aje?***
Niko hapa saa kumi na mbili na robo asubuhi 6:15 a.m. kwa wale wanafunzi wanao letwa kabla ya chakula cha asubuhi kuanza, na kuanzia hapo tuko tayari kazini! Tuna maingiliano na familia na wanafunzi siku nzima na kila siku kuna changamoto mpya za kudhibiti. Mwanafunzi alisahau chakula chake cha mchana, mtu fulani anapitia hali ngumu nyumbani, taja jambo lolote, tuko hapa kufanya siku iwe bora zaidi. Nadhani wafanyakazi wa ofisini ni kama gundi la jengo – tunasaidia kushikilia vitu vingi pamoja. Shule ni kama familia ya pili kwa watu wanaofanya kazi hapa na kwa wanafunzi. Nimekuwa hapa miaka 21 na kwa hivyo najua vile ni muhimu kujenga mahusiano hayo na watu.

> "Hii ni zaidi kuliko shule pekee. Sisi ni familia. Sote tuko hapa tukifanya kazi mambo yaende vyema na kuweka watoto wetu salana na wasome."

***Ni jambo gani una jivunia nalo sana?***

Napenda ukweli wa kwamba watoto wanaweza kuja kuniona kuhusu jambo lolote, hata kama wanahitaji mapumziko ya dakika tano. Wananifahamu kama Bi. Sandra. Katika shule ya kati nafasi hiyo salama ni muhimu sana. Kuna mabadiliko mengi na inaweza kuwa ni marekebisho makubwa kwa watoto. Sio kila mtu ako na maisha bora nyumbani. Kwa hivyo kwa wanafunzi, kufahamu wako salama na ya kwamba wako na mtu wanao weza kuogelesha ikiwa wamekosana na rafiki au jambo limetendeka nyumbani, hii inaleta tofauti kubwa. Najivunia kushiriki kwa hayo.

***Je, ungependa watu wengi kujua nini kuhusu kazi yako?***
Sijui kama watu wanatambua mambo mengi tunayo fanya katika ofisi ya shule. Ni zaidi sana kuliko kujibu simu tu. Huu ni wakati ambapo tuko na shughuli nyingi mno, na tunaweza hitaji sekunde kukamilisha jambo moja kabla ya kwenda kwa jambo jingine. Lakini kwa kila mtu katika jengo hili, kwa uhakika ni "mtoto kwanza." Hii ni zaidi kuliko shule pekee. Sisi ni familia. Sote tuko hapa tukifanya kazi mambo yaende vyema na kuweka watoto wetu salana na wasome. Naelewa ya kwamba saa zingine kuna mfadhaiko kwa sababu wazazi wanajali zaidi kuhusu watoto wao. Nililea mtoto wa kike na niko na huruma. Lakini natumaini ya kwamba wanafahamu tuko hapa kusaidia, na hawa watoto ni muhimu mno kwetu.

***Je, unatarajia nini mwaka ujao?***

Tuko na maelekezo wiki hii na ningependelea kuona nyuso hizi zote nzuri! Wako na hamu kuu ya kurudi shuleni. Katika mwanzo wa mwaka, isipokuwa kama ulikuwa kwa shule ya kati, ni vigumu kuelezea. Wanafunzi wa darasa la sita wana mambo mengi ya kuzingatia, na tuna hakikisha ya kwamba tuko hapa kuwasaidia. Tunajenga uhusiano huo. Watoto wanakaa nasi na tunakula chakula cha mchana, ina saidia kuwajulisha ya kwamba watakuwa sawa. Na baada ya wiki chache za kwanza tunaingia katika utaratibu. Watakuwa na wasiwasi mwanzoni, lakini watoto wanahisi vizuri sana baada ya kazoea. Hii ni jambo zuri sana la kuona.

## NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI


- Shule ya Msingi ya D'Abate Elementary katika Providence ikipata marekebisho yalio chelewa kufanywa
  Jarida la Providence, Agosti 11
- Shule za Umma za Providence zina tambuliwa katika bidii za eletroniki za kudumu
  habari za Biashara za Providence, Agosti 9
- Mipango ya Kabla ya Vyuo ya Brown inakaribisha idadi kubwa ya wanafunzi kutoka
  Chuo Kikuu cha Providence Brown, Agosti 8
- Idara ya kuzima moto ya Providence inapeana wanafunzi jaribio katika kazi
  Jarida la Providence, Agosti 4
- Shule ya Kati ya Middle inakusanya, na kugawa mamia ya madoli kwa wanafunzi wa Uvalde
  WJAR, Julai 26

## WILAYANI



### MAFANIKIO YA MAJIRA YA JOTO

Majira haya ya joto, takriban wanafunzi 3,000 wa Shule ya Umma ya Providence walishiriki katika **mafunzo ya majira ya joto** katika madarasa ya K-12! Wanafunzi hadi darasa la 8 walishiriki kwa madarasa yanayo angazia Sanaa ya Lugha ya Kiingereza, Hesabu, Sayansi na ujuzi wa STEM. Wanafunzi wa Shule ya Upili wanaweza kushiriki katika upataji wa alama na Elimu ya Kazi na Ufundi (CTE). Asante kwa mamia ya wafanyakazi na walimu ambao wametusaidia kuziba pengo la mafanikio na kuhudumia wanafunzi wetu mwaka mzima.




### KUBORESHA MAENDELEO YA KITAALUMA YANAYOHITAJIKA

Majira haya ya joto ni wakati wa walimu wa PPSD kukusanyika na kujifunza njia mpya za kusaidia wanafunzi kupokea mafanikio. Ndani ya wiki kadhaa zilizopita, Wilaya iliandaa **Akademia ya Viongozi Wapya** kwa Maofisa Wakuu Wasaidizi wa Wasimamizi na Wakurugenzi Watendaji, akademia ya wiki mbili ya Walimu Wakuu, akademia ya Wakufunzi, akademia ya wiki mbili ya Mwalimu Mpya, na Akademia ya Mwalimu yenye vikao zaidi ya 100 vya maendeleo ya kitaaluma.



### IMETENGENEZWA KATIKA KIVULI

Asante kubwa kwa mshauri wa muda mrefu wa **Aramark** Bob Struck, ambaye hivi majuzi ali lipia kupata kivuli vipya viwekwe kwenye ghorofa ya kwanza ya **Shule ya Msingi ya Robert F. Kennedy**! Mwanga wa jua kali ulikuwa ni tatizo sehemu hii ya mjengo. Kwa hivyo Bob, ambaye mamake alikuwa mwalimu katika Shule ya Msingi ya Kennedy na ambaye watoto wake wasichana wanne wote walihudhuria shule hiyo, ali lipia vivuli mwenyewe na kuviweka!



### KUVUNJA ARDHI MPYA

Mwezi huu, ujenzi ulianza na urekebishaji wa milioni $21 wa **Shule ya Msingi ya William D'Abate**. Ubadilishaji huu kamili uta tengeneza mazingira ya kisasa, ya karne ya 21 ya masomo ambayo yatachangia mafanikio ya elimu na ukuaji wa kijamii na kiakili kwa wanafunzi. Ujenzi unaendelea mwaka wa shule wote wa 2022-23, ikiwa na wanafunzi wa D'Abate na wafanyakazi wamepewa makazi ya muda katika shule ya msingi ya Lauro iliyo karibu.

## WEKA ALAMA KWA KALENDA YAKO!


- **WAFANYAKAZI KURUDI KWA MAENDELEO YA KITAALUMA**
  Jumatatu, Agosti 22, 2022
- **SIKU YA MSINGI YA UCHAGUZI**
  (HAKUNA SHULE)
  Jumanne, Septemba 13, 2022
- **SIKU YA KWANZA YA MADARASA**
  Jumatatu, Agosti 29, 2022
- **MASAA 2-KUACHISHWA MAPEMA**
  Jumatano, Septemba 21, 2022
- **SIKU YA WAFANYAKAZI**
  *(HAKUNA SHULE)*
  Jumatatu, Septemba 5, 2022
- **ROSH HASHANAH** *(HAKUNA SHULE)*
  Septemba 26 & 27, 2022




### BEGI ZA BURE NA BIDHAA ZA SHULE

**Jumamosi, Agosti 27**
**Saa nne asubuhi hadi saa sita mchana (10:00 a.m -12:00 p.m)**
**Tukio la Kuingia na Gari**
**Sehemu Nyingi ikiwemo:**

- Providence Community Health Center, 31 Atwood St.
- West End Community Center, 109 Bucklin St.
- Providence Information & Student Registration, 325 Ocean St.
- Nathanael Greene Middle School, 721 Chalkstone Ave.




### MT. PLEASANT SIKU YA KUREMBESHA

**Jumamosi, Agosti 20**
**Saa tatu asubuhi hadi nne usiku (9:00 a.m -10:00 p.m)**

Jiunge nasi Jumatano hii, Agosti 20, kwa Siku ya Kurembesha katika Shule ya Upili ya Mount Pleasant! Siku itaanza na matembezi ya shule kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa nne asubuhi (9-10 a.m). Baada ya hii itakuwa kupeana zawadi na mazungumzo ya jumuiya, iki fuatwa na kazi za bustani kurembesha uwanja wa shule. Wanajumuiya wote wana karibishwa kuhudhuria kwa siku kadhaa au siku zote!

### MANUFAA YA WAFANYAKAZI!

**DSW Inapunguza bei ya Wafanyakazi wa PPSD**
Makini kwa wafanyakazi wa PPSD – tumia ofa iliyofunganishwa kutoka DSW *(Designer Shoe Warehouse)* kutoka Agosti 26 hadi 28 na upate upunguzaji wa 20% kwa bei ya kawaida ya bidhaa na ziada ya upungufu wa 10% wa kumalizia bidhaa! Hakikisha kupata kipeperushi hiki na kitambulisho cha mfanyakazi katika sehemu ya kutoka kupokea upunguzaji wa bei.

**Bom Bom Nutrition Inapunguza bei ya Wafanyakazi wa PPSD**
Wafanyakazi wa PPSD wanaweza pia kupokea upunguzaji wa bei maalum kutoka Bom Bom Nutrition katika 375 Washington Street kupitia mwisho wa Agosti. Tazama picha iliyounganishwa kwa mipango ya kila siku, na kuhakisha uko na kitambulisho chako cha Shule za Umma za Providence katika sehemu ya kutoka.

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima, na tunataka kueneza ujumbe! Ikiwa una programu, tukio, mfanyakazi, au mwanafunzi mwenye hadithi ya kushangaza ambayo ungependa kuangazia, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.

Providence Schools

© 2022 Shule za Umma za Providence · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org